K.P.S.E.A
TATHMINI YA SHULE YA MSINGI
KAZI YA AGOSTI, 2026
GREDI YA 6 -

KISWAHILI KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA
Muda: 20 KILA MWANAFUNZI

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

Jina: ______________________________ Shule: ______________________________

Nambari ya Tathmini: ______________________________ Tarehe: ______________________________

Nambari ya Shule: ______________________________ Sahihi: ______________________________

**MAELEKEZO KWA WANAFUNZI**

1. Andika jina lako, jina la shule yako na nambari yako ya mthani katika nafasi ulizoachiwa.
2. Andika tarehe,nambari ya shule yako kisa weka sahihi yako.
3. Soma kila swali kwa makini
4. Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote kwenye kijitabu hiki zimepigwa chapa.
5. Soma kifungu ulichopewa

**JEDWALI LA ALAMA**

| SEHEMU | INSHA | LUGHA | KUSI/KUZU | ASILIMIA (%) | KUZ 1 | KUZ 2 | KUF 1 | KUF 2 | KUK 1 | KUK 2 | CHI 1 | CHI12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KIWANGO CHA ALAMA | ALAMA 20 | ALAMA 30 | ALAMA 30 | | 90-100 | 75-89 | 58-74 | 41-57 | 31-40 | 21-30 | 11-20 | 1-10 |
| POINTI | | | | | 8 POINTI | 7 POINTI | 6 POINTI | 5 POINTI | 4 POINTI | 3 POINTI | 2 POINTI | 1 POINTI |
| JUMLA YA ALAMA ZA MWANAFUNZI | | | | | | | | | | | | |

# JUMA NA SIKU YA MVUA KALI

Ilikuwa siku ya Jumanne asubuhi katika kijiji cha Amani. Anga lilikuwa limejaa mawingu mazito na upepo mkali ulivuma kila upande. Wanafunzi walikuwa wakijiandaa kwenda shuleni huku wakihisi kuwa mvua ingeshaanza muda wowote.

Juma, mwanafunzi wa Gredi ya 5, aliondoka nyumbani akiwa amebeba begi lake na mwavuli mdogo. Alikuwa mtoto mnyenyekevu, mchangamfu na aliyependa kusaidia wengine. Kila siku alipenda kufika shuleni mapema ili asikose mazoezi ya asubuhi.

Alipokuwa akipita karibu na daraja la kijijini, mvua kubwa ilianza kunyesha kwa ghafla. Maji yaliongezeka barabarani na upepo mkali ulivunja matawi ya miti. Watu wengi walikimbia kujificha.

Juma aliona mwanafunzi mdogo wa darasa la tatu akiwa amesimama pembeni analia kwa sababu hakuweza kuvuka maji yaliyokuwa yamejaa barabarani. Bila kusita, Juma alimshika mkono na kumsaidia kutafuta njia salama ya kuvuka.

Baada ya muda mfupi, walifanikiwa kufika upande mwingine kwa usalama. Mvulana huyo alimshukuru Juma kwa kumsaidia wakati mgumu. Juma alitabasamu na kusema, “Ni vizuri kusaidiana wakati wa shida.”

Wakiwa bado njiani, walikutana na dereva wa pikipiki ambaye pikipiki yake ilikuwa imekwama kwenye matope. Juma alisaidia kusukuma pikipiki hadi ikatoka kwenye matope hayo.

Baada ya muda, mvua ilipungua na jua likaanza kuchomoza. Wanafunzi walifika shuleni wakiwa wamechelewa kidogo, lakini walipokelewa vizuri na mwalimu wao.

Mwalimu aliposikia kuhusu msaada wa Juma, alimpongeza mbele ya darasa lote. “Umeonyesha mfano mzuri wa upendo na ushirikiano,” alisema mwalimu.

Wanafunzi wote walimshangilia Juma kwa makofi. Juma alijisikia furaha moyoni kwa sababu alisaidia wengine bila kutarajia chochote.

Tangu siku hiyo, Juma alijulikana kijijini kama mtoto mwenye moyo wa huruma na msaada kwa wengine.

# HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA

# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA (JUMLA: ALAMA 30)

## 1. Ufasaha wa Kusoma (Fluency) – Alama 15

| Kiwango | Maelezo | Alama |
|---|---|---|
| Aya ya 1 | Anasoma kwa shida sana | 3 |
| Hadi Aya ya 2 | Anasoma sentensi fupi | 6 |
| Hadi Aya ya 3 | Anasoma kwa wastani | 9 |
| Hadi Aya ya 4 | Anasoma vizuri | 11 |
| Hadi Aya ya 5 | Anasoma kwa ufasaha mzuri | 13 |
| Aya zote | Ufasaha wa juu kabisa | 15 |

## 2. Matamshi na Usahihi – Alama 10

| Kiwango | Maelezo | Alama |
|---|---|---|
| Dhaifu | Makosa mengi | 2–3 |
| Wastani | Makosa machache | 4–5 |
| Nzuri | Sahihi kwa kiasi kikubwa | 6–7 |
| Nzuri sana | Karibu sahihi yote | 8–9 |
| Bora sana | Sahihi kabisa | 10 |

## 3. Ujasiri na Mtindo wa Kusoma – Alama 5

| Kiwango | Maelezo | Alama |
|---|---|---|
| Chini | Hana ujasiri | 1 |
| Wastani | Kidogo ujasiri | 2 |
| Nzuri | Ujasiri kiasi | 3 |
| Nzuri sana | Ujasiri mzuri | 4 |
| Bora sana | Ujasiri mkubwa | 5 |